

**MKATABA WA KUKODISHA ENEO LA UCHIMBAJI WA MAWE
YANAYOSADIKIWA KUWA NA DHAHABU**

KATI YA

IGALULA GOLD MINE

(MMILIKI WA ENEO)

NA

ZHONG TAN SHUN KUN MINING COMPANY LIMITED

(MWEKEZAJI)

**Mkataba huu umeandaliwa na;
Penina Mashimba - Wakili
Mana and Company Advocates
Soko la Dhahabu nearby Nyehunge pharmacy
Mobile: 0758 899 151/0767893880
S.L.P 254
Mwanza
[Email:peninamashimba254@gmail.com](mailto:peninamashimba254@gmail.com)**

**MKATABA WA KUKODISHA ENEO LA UCHIMBAJI WA MAWE YANAYOSADIKIWA
KUWA NA DHAHABU**

Mkataba huu unatiwa saini leo tarehe 13 mwezi Mei, 2024 kati ya **IGAGULA GOLD MINE** Mgodi wa uchimbaji madini uliosajiriwa kisheria wenye Sanduku la Posta 116 Kahama - Shinyanga, (katika mkataba huu Inajulikana kama **'MMILIKI WA ENEO**) kwa upande mmoja: **NA ZHONG TAN SHUN KUN MINING COMPANY LIMITED** Kampuni binafsi Iliyosajiliwa chini Sheria ya Makampuni ya Tanzania (**The Companies Act Cap. 212 (RE) 2002**) yenye namba za usajiri **174525218**, na yenye Sanduku la Posta **384** Geita (ambayo katika mkataba huu inajulikana kama **'MWEKEZAJI'**) kwa upande mwingine.

KWAMBA, Wamiliki wameamua kumkodishia Mwekezaji eneo lao uchimbaji wa dhahabu lililopo Wilaya ya Nyang'hwale Mkoani Geita - Tanzania kupitia leseni za uchimbaji namba **PML0395GTA, 0396GTA, 0397GTAGTA, 0398GTA** na **0399GTA**, kwa masharti na gharama iliyoelezwa ndani ya mkataba huu;

NA KWAMBA, Mwekezaji ameamua kwa hiari yake kuingia kwenye makubaliano haya ya uchimbaji wa dhahabu katika eneo la Wamiliki kwa masharti na maelekezo kama yalivyoenezwa ndani ya mkataba huu;


HIVYO BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA KAMA IFUATAVYO;


1. **KWAMBA** Wamiliki wa eneo wanamkodisha Mwekezaji eneo lao uchimbaji wa dhahabu lililopo Wilaya ya Nyang'hwale Mkoani Geita - Tanzania kupitia leseni za uchimbaji namba **PML0395GTA, 0396GTA, 0397GTAGTA, 0398GTA** na **0399GTA**.
2. **KWAMBA WAMILIKI WA ENEO** na **MWEKEZAJI** wanakubaliana kuwa, baada ya zoezi zima la uchimbaji na uzalishaji wa dhahabu kukamilika, watatoa malipo yote ya Serikali ambayo ni ada ya mrahaba (**royalty**), ukaguzi, TRA na ushuru wa huduma (**Service Levy**) na kisha kiasi cha fedha kitakachobaki kitagawanywa katika asilimia zifuatazo **MMILIKI WA ENEO** atapata asilimia Kumi na Sita (**16%**) na **MWEKEZAJI** Asilimia themanini na nne (**84%**).
3. **KWAMBA MMILIKI WA ENEO** na **MWEKEZAJI** wanakubaliana kwamba jukumu la ulipaji ya kodi ya Serikali pamoja na kutambua wamilikiwa leseni ya uchimbaji katika eneo linalochimbwa litakuwa jukumu la **MWEKEZAJI** na kufuata sheria za Nchi za uchimbaji.

4. KWAMBA MMILIKI WA ENEO hawatambugudhi na kumwingilia MWEKEZAJI endapo anatekeleza makubaliano na kufuata sheria za uchimbaji.
5. KWAMBA Mwekezaji atahakikisha anatoa huduma za kijiji na kwa jamii inayowazunguka kwa muda watakaokuwa wamepanga na kutoa ushirikiano na mwenyekiti wa kijiji na mtendaji wa Serikali ya kijiji pale utakapohitajika msaada kwake pamoja na gharama za wageni kutoka serikalini.

HIVYO BASI kwa pande zote mbili kusaini mkataba huu, zitahakikisha zinaheshimu na kulinda masharti yaliyoelezwa ndani ya mkataba huu.


Umetiwa saini na kutolewa Geita na IGALULA GOLD MINE leo hii tarehe¹³
mwezi⁰⁵..... 2024

Jina: JUMANWE SENOD MIAUNGWI
Saini: 
Anuani: 116 KAHAMA
Wadhifa: MWENYEKITI
Tarehe: 13/05/2024



Jina: HUSSEIN MAKUBI NAGA
Saini: 
Anuani: 116 KAHAMA
Wadhifa: MWENYEKITI
Tarehe: 17/05/2024



Jina: DAVID NDUU MACAMBA
Saini: 
Anuani: 116 KAHAMA
Wadhifa: MWENYEKITI
Tarehe: 13/05/2024



Umetiwa saini na kutolewa Geita na ZHONG TAN SHUN KUN MINING COMPAI LIMITED leo hii tarehe ..13..... mwezi05..... 2024

Jina: ..DK XINMING.....
Saini:
Anuani: SLP 384 GEITA
Wadhifa: MUKUBENZI
Tarehe: 13.05.2024



Jina: ..IAN XIAO FENG.....
Saini:
Anuani: SLP 384 GEITA
Wadhifa: MUKUBENZI
Tarehe: 13.05.2024

MAKATABA HUU UMESAINIWA MBELE YA WAKILI:

Jina: ..PENINA MASHAUSA.....
Saini:
Anuani: SLP 254 - MASHAUSA
Tarehe: 13.05.2024

